
NYARAKA 2

COMIC BIBLE
SOCIETY

Published by the Comic Bible Society, LLC
Copyright © 2023

Kingstone Comics maintains copyright to this comic book as provided by United States copyright law.

Print and digital copies of this version may be freely distributed without penalty under a Creative Commons license.



WAFILIPI
KANISA HUKO KWENYE KOLONI YA KIROMA YA FILIPI ILIANZISHWA NA PAULO KWA SAFARI YAKE YA PILI YA KIMISHONARI.
HAPO, ALIMTOA PEPO KUTOKA KWA MSICHANA ALIYEPIGA RAMLI, ILIYOSABABAISHA KUTANDIKWA NA KUFUNGWA KWAKE.
ALIPOKUWA GEREZANI ROMA ALIPOKEA ZAWADI KUTOKA KWA KANISA LA FILIPI.
KILA KILICHONITENDEKEA KIMENISAIDIA KUIENEZA HABARI NJEMA YA KRISTO.
KWA SABABU YA KUFUNGWA KWANGU WENGI WA WAKRISTO WAMEKUWA NA UJASIRI WA KUWAAMBIA WENGINE KUMHUSU.
WENGINE WAMHUBIRI KRISTO KWA SABABU WANANIONEA WIVU, ILHALI WENGINE WANAMHUBIRI KRISTO KWA NIA NJEMA.
HAIJALISHI NIA YAO - KRISTO AHUBIRIWA, NAMI NAFURAHIA.
CHOCHOTE KITAKACHOTOKEA, ISHINI KAMA WAKRISTO, ILI KAMA NITAWAONA TENA AU NITASIKIA TU KUWAHUSU, NITAJUA KUWA MUNASIMAMA IMARA NA NIA MOJA - KUISEMA HABARI NJEMA.



"IJALIZENI FURAHA YANGU KWA KUPENDANA NA KUELEWANA, MKIFANYA KAZI PAMOJA KWA MOYO NA AKILI NA NIA MOJA."
"MSIWE NA UBINAFSI ILA MUWE WANYENYEKEVU, MKIWAWAZA WENZENU BORA ZAIDI YENU."
"MTAZAMO WENU UNASTAHILI KUWA KAMA WA YESU KRISTO, AMBAYE, INGAWA ALIKUWA MUNGU, HAKUDAI HAKI YAKE KAMA MUNGU ILA ALIWEKA KANDO NGUVU ZAKE NA UTUKUFU, AKAWA KAMA MTUMWA NA KUUCHUKUA MFANO WA BINAADAM."
"NA ALINYENYEKEA ZAIDI, HATA KUFA KIFO CHA MHALIFU KWENYE MSALABA."
"YATENDENI MAMBO YOTE PASIPO MANUNG'UNIKO NA MASHINDANO."
"JITAHADHARINI NA WALE WANAUME WAOVU--MBWA HATARI, NINAVYOWAITA--WASEMAO LAZIMA MPASHWE TOHARA ILI MUOKOKE."
"KAMA YEYOTE ANGEONA ANA SABABU YA KUTUMAINI AWEZA KUJIOKOA MWENYEWE, NI MIMI."
DANNY BULANADI/17



"KAZALIWA KWENYE KABILA LA BENYAMINI, MMOJAWAPO WA MAFARISAYO. NILIITII KILA SHERIA YA KIYAHUDI KWA DHATI NA KULITESA KANISA."
"LAKINI MAMBO YALE YALIYOKUWA FAIDA KWANGU-NIMEYATUPA KANDO ILI NIWEKE IMANI NA TUMAINI LANGU NDANI YA KRISTO PEKEE."
"NAAM, YOTE NI HASARA YAKILINGANISHWA NA MANUFAA MARADUFU YA KUMJUA KRISTO YESU BWANA WANGU."


"FURAHINI KATIKA BWANA SIKU ZOTE; TENA NASEMA, FURAHINI!"
"ACHENI KILA MMOJA AONE KUWA HAMNA UBINAFSI NA MWAJALI KWA YOTE MNAYOYATENDA."
"MSISUMBUKE KWA NENO LOLOTE; BALI, KWA KILA JAMBO OMBENI."
"NINAPOIFUNGA BARUA HII, ACHA NISEME KITU KIMOJA ZAIDI - TAFAKARINI YALIYO KWELI NA YA KUPENDEZA NA YA HAKI."
"TAFAKARI YOTE MNAYOWEZA KUMSIFU MUNGU KUHUSU NA KUFURAHIKIA."
"SIVYO NINAVYOMSHUKURU NA KUMSIFU BWANA KWA KUWA MWANISAIDIA TENA."
"NIMEJIFUNZA SIRI YA KUWA RADHI NA HALI YOYOTE NILIYO NAYO...KWA KUWA NAYAWEZA MAMBO YOTE MUNGU ANIULIZA NIFANYE NA USAIDIZI WA KRISTO."
"SALIMIENI KILA MTUKUFU KATIKA KRISTO YESU - WATAKATIFU WOTE HAPA WAWASALIMU - HASA WAFANYIKAZI NYUMBANI MWA KAISARI."


WAKOLOSAI
KOLOSAI ULIKUWA MJI HUKO FRIGIA (SASA HIVI UTURUKI) NA KAMA MAILI 100 MASHARIKI MWA EFESO.
MTUME PAULO HAKULIANZISHA KANISA HILI, LILIPANDWA NA MWANAUME JINA LAKE EPAFRA ALIYEOKOKA CHINI YA HUDUMA YA PAULO KULE EFESO.
KANISA LILIPITIA UZUSHI MARA MBILI - MOJA, KUWA YESU ALIKUWA CHINI YA MUNGU NA ILIWABIDI WATU KUTAFUTA UJUZI WA JUU ZAIDI KULIKO MAANDIKO KWA KUELIMIKA.
YA PILI ILITOA WITO KWA IBADA YA MALAIKA NA KUFUATIA SHERIA ZA KIYAHUDI KWA AJILI YA UOKOVU.
AKIANDIKA KUTOKA JELA YAKE HUKO ROMA, PAULO ALIYAGUSIA YOTE MAWILI HAYA.
"KRISTO NI MFANO WA MUNGU ASIYEONEKANA. ALIKUWEPO KABLA MUNGU AUMBE CHOCHOTE."
"KRISTO NI MUUMBAJI ALIYEUMBA KILA KITU MBINGUNI NA DUNIANI - TUNAVYOVIONA NA TUSIVYOWEZA KUVIONA."
"ALIKUWEPO KABLA YOTE MENGINE YAANZE NA NI NGUVU ZAKE ZISHIKILIAZO KILA KITU PAMOJA."
"NAYE NDIYE KICHWA CHA MWILI - YAANI, KANISA LAKE."


"NAJITAHIDI KUWAOMBEA - ILI MUMJUE KRISTO NA KUMFAHAMU FIKA."
"NDANI YAKE MUMEFICHWA HAZINA ZOTE ZA HEKIMA NA UJUZI."
"NAOGOPA MTU ANAWEZA KUWAHADAA NA MDOMO MTAMU."
"ZINGATIENI KUWA MUENDELEE KUA KATIKA BWANA NA KUA WENYE NGUVU KATIKA UKWELI MLIOFUNZWA."
"MUSIACHE WENGINE WAHARIBU IMANI NA FURAHA YENU NA FALSAFA ZAO ZILIZO NA MSINGI KWA MAWAZO YA WANAADAMU."
"KWANI KATIKA YESU KUNA MUNGU WOTE KWENYE MWILI WA MWANAADAMU - ANA MAMLAKA JUU YA NGUVU ZOTE."
"MLIKUWA WAFU KATIKA DHAMBI, KISHA AKAWAPA USHIRIKI KATIKA MAISHA YA KRISTO, KWANI ALIZISAMEHEA DHAMBI ZENU ZOTE."
"TANGU MFE NA KRISTO KWA MAWAZO YA DUNIA JINSI YA KUOKOKA - MBONA MWAENDELEA TU KUFUATA SHERIA HIZI ZA KUTOKULA, KUTOONJA, AMA HATA KUTOGUSA VYAKULA FLANI?"


"SASA MKO HAI NA KRISTO, TAZAMENI UTAJIRI WA HAZINA NA FURAHA ZA MBINGUNI ANAPOKAA UBAVUNI MWA MUNGU MAHALI PA HESHIMA NA NGUVU."
"TUPA HAMU ZA DHAMBI NA MSIHUSIKE KABISA NA DHAMBI YA NGONO, UCHAFU, TAMAA, NA MATAMANIO YA AIBU."
"VUENI NGUO ZA HASIRA, CHUKO, KULAANI NA LUGHA CHAFU."
"MSIDANGANYANE KAMA MAISHA YENU YA MBELENI ILA JIFUNZENI KILICHO HAKI - MKIJARIBU KUWA ZAIDI KAMA KRISTO."
"MAANA MUMECHAGULIWA NA MAPENZI TELE YA MUNGU - MUWE NA VITENDO VYA UPENDO NA UKARIMU KWA WENZENU."
"MUWE WAPOLE NA WALIO TAYARI KUSAMEHE; MSIWE NA KINYONGO."
"KUMBUKENI ALICHOFUNZA KRISTO, NA ACHENI NENO LAKE LIYATAJIRISHE MAISHA YENU NA KUWAPA HEKIMA."
"NA KILA MNACHOKITENDA AU KUSEMA - ACHENI KIWE KAMA MWAKILISHI WA BWANA YESU."






WAKOLOSAI 3:18-4:18


BAADA YA KUTESWA [1] HUKO FILIPI, PAULO ALISAFIRI KWENDA THESALONIKE, MJI MKUU WA MAKEDONIA, ALIKOPANDA KANISA.
I, II WATHESALONIKE
KUTOKA KORINTHO MNAMO 51 A.D. ALIANDIKA BARUA YAKE YA PILI YA KANUNI.
KILA TUENDAPO TWAPATA WATU WAKITUAMBIA KUHUSU IMANI YENU YA AJABU NDANI YA MUNGU.
[1] MATENDO 16
BAADA YA KUTUSIWA HUKO FILIPI, MUNGU ALITUPA UJASIRI KUREGELEA UJUMBE HUO KWENU.
KWANI TWAZUNGUMZA KAMA WAJUMBE WAAMINIFU KUTOKA KWA MUNGU, HATUBADILIKI KULINGANA NA WANAOSIKIZA.
"KUMBUKA TULIVYOFANYA KAZI USIKU NA MCHANA ILI GHARAMA ZETU ZISIWE MZIGO KWA YEYOTE TULIPOHUBIRI HABARI NJEMA YA MUNGU KATI YENU."
"BAADA YA KUWA MBALI NANYI ILA KWA MDA MFUPI TULIJARIBU KURUDI LAKINI IBILISI ALITUZUIA."
"KWANI NI NINI TUZO LETU LA FAHARI NA TAJI? NI NYINYI!"


"NILIPOSHINDWA NILIMTUMA TIMOTHEO AWATIE MOYO - NILIOGOPA KUWA IBILISI ALIWAZIDI NGUVU NA KAZI YETU ILIKUWA IMEAMBULIA PATUPU."
"LAKINI TIMOTHEO ALIRUDI NA UJUMBE KUWA IMANI NA UPENDO WENU NI WENYE NGUVU ZAIDI NA KUWA MWATUKUMBUKA NA FURAHA - KWA HIYO SASA TUMETIWA MOYO."
"NA MUNGU AFANYE UPENDO WENU UKUE NA KUMWAGIKA KWA WENZENU NA KWA WENGINE WOTE, KAMA UPENDO WETU KWENU UFANYAVYO."
"MUNGU ATAKA MJIEPUSHE NA KUZINI ILI KILA MMOJ WENU AOE KATIKA UTAKATIFU NA HESHIMA - NA MSICHUKUE WAKE WA WAUME WENGINE - MUNGU ATAWAADHIBU VIKALI KWA HILI."
"NATAKA MUJUE KINACHOTENDEKA MKRISTO ANAPOKUFA - ILI MSIHUZUNIKE KAMA WASIO NA TUMAINI."
"MAANA YESU ALIKUFA NA KURUDI HAI TENA, ATAKAPOREGEA MUNGU ATARUDI NA WAKRISTO WOTE WALIOKUFA."




I WATHESALONIKE 4:15-5:28






II WATHESALONIKE 1:1 - 2:3


" SIKU HIYO HAIJI MPAKA KUWE NA UASI MKUU DHIDI YA MUNGU, KISHA MWANA WA JAANAM ATAKUJA."
"ATAKATAA MIUNGU YOTE ILIYOKO NA KUENDA KWA HEKALU YA MUNGU - AKIDAI KUWA YEYE MWENYEWE NI MUNGU."
"YULE MTU WA UASI HATAKUJA MPAKA YULE ANAYEMZUIA ATAKAPOONDOKA."
"KISHA HUYU MUOVU ATATOKEA, AMBAYE BWANA YESU ATAMCHOMA NA PUMZI YA KINYWA CHAKE NA KUMHARIBU KAWA UWEPO WAKE ATAKAPORUDI."
"MTU HUYU WA DHAMBI ATAKUJA NA NGUVU ZA KISHETANI NA KUWALAGHAI KILA MMOJA NA MAONYESHO YA AJABU NA MIUJIZA MIKUU."
"ATAWALAGHAI WALIOPOTEA KWA SABABU WAMEKATAA KUAMINI UKWELI."
"MKIYAZINGATIA HAYA YOTE, NDUGU WAPENDWA, SIMAMENI WIMA NA MUUSHIKILIE KWA NGUVU UKWELI TULIOWAFUNZA KWENYE BARUA ZETU NA WAKATI TULIPOKUWA NANYI."
II WATHESALONIKE 2:3-15



"HATIMAYE, NAWAOMBA MUOMBE NASI KUWA NENO LA BWANA LITAENEA KWA KASI, LIKIWABADILISHA WENGI KAMA LILIVYOFANYA TULIPOKUJA KWENU."
"OMBENI KUWA TUTAOKOLEWA KUTOKA KWA MIKONO YA WATU WAOUVU, KWANI SIO KILA MTU ALIE NA IMANI."
"LAKINI BWANA NI MUAMINIFU - ATAWAPA NGUVU NA KUWALINDA KUTOKA MASHAMBULIZI YA IBILISI."
"HII NI AMRI ILIYOPEWA KWA MAMLAKA YA KRISTO - KAENI KANDO NA MKRISTO YEYOTE ANAYESHINDA KWA UVIVU NA ASIYEFANYA KAZI KWA BIDII."
"MWAFAA KUUFUATA MFANO WETU - TULIFANYA KAZI KWA BIDII WALA HATUKU-CHUKUA CHAKULA KUTOKA KWA YEYOTE BILA KUKINUNUA - ILI TUSIWALEMEE."
"KWA WALE WALIO WAVIVU NA NA WAMBEA - TUNAWAAMURU WATENDE KAZI KWA UTULIVU NA KUTAFUTA MAPATO YAO WENYEWE."
"NA KWA WENGINE NASEMA - MSICHOKE KUTENDA MEMA."
"BARAKA YA BWANA WETU YESU KRISTO IWE NA NYINYI NYOTE."


TIMOTHEO ALOKUWA KIJANA MDOGO KATIKA KITONGOJI CHA GALATIA (UTURUKI WA LEO) AMBAYE MTUME PAULO ALIMUONGOZA KWA KRISTO KWENYE SAFARI YAKE YA KWANZA YA UMISHONARI.
I, II TIMOTHEO
PAULO ALIENDA PAMOJA NA TIMOTHEO KWENYE SAFARI YAKE YA PILI YA KIMISHONARI.
TIMOTHEO ALIKUWA KIJANA MCHA MUNGU, NA AKAWA MCHUNGAJI WA KANISA HUKO EFESO.
ALIPOACHILIWA KUTOKA KIFUNGO CHAKE CHA KWANZA HUKO ROMA, WALIPOENDA NA LUKA, PAULO ALIANDIKA BARUA YAKE YA KWANZA KWA TIMOTHEO.
"KWA TIMOTHEO, MWANANGU HASA KATIKA IMANI - NAKUSIHI IKAE EFESO ILI UWAKATAZE WENGINE WASIFUNDISHE ELIMU NYENGINE."
"NAMSHUKURU SANA YESU KRISTO BWANA WETU KWA KUNICHAGUA MIMI HATA KAMA NILIWADHURU WATU WAKE."
"NI NENO LA KUAMINIWA KUWA KRISTO ALIKUJA DUNIANI KUWAOKOA WENYE DHAMBI - AMBAO WA KWANZA WAO NI MIMI."
"TIMOTHEO, MWANANGU, PIGANA VYEMA KWENYE VITA VYA BWANA [1] NA SIKU ZOTE UWE NA DHAMIRA NJEMA."
[1] TIMOTHEO ALIFUATA AMRI ALIYOPEWA. ALIPIGWA MPAKA AKAFA NA UMATI HUKO EFESO KWA KUHUBIRI DHIDI YA MUNGU WA KIKE DIANA.


"WAOMBEENI WAFALME NA WENYE MAMLAKA ILI TUISHI KWA AMANI NA UTULIVU."
"HILI NI ZURI NA LAKUBALIKA MUNGU MKOMBOZI WETU AMBAYE HUTAKA WATU WOTE WAOKOKE NA KUPATA KUUJUA UKWELI WAKE."
"NATAKA WANAUME KILA MAHALI WASALI HUKU WAKIINUA MIKONO ILIYOTAKATA KWA MUNGU."
"NA WANAWAKE WAKRISTO WAONEKANA KWA AJILI YA KUWA WAKARIMU NA WEMA, SIO KWA NAMNA WAKIOTENGENEZA NYWELE ZAO AU KWA JOHARI AU NGUO ZA THAMANI."
"IMEMPASA ASKOFU AWE MWANAMUME MWEMA AMBAYE SIO MKRISTO MPYA NA AMBAYE HANA BAYA LA KUSEMWA DHIDI YA MAISHA YAKE."
"ANAFAA AWE MUME WA MKE MMOJA NA JAMII NJEMA ILI AWEZE KUONGOZA KANISA."
"HIVYO HIVYO MASHEMASI WAWE WEMA VILE VILE, WASTAHIVU KAMA MAASKOFU. SI WATU WA KUTUMIA MVINYO SANA NA SIO WATU WANAOTAMANI FEDHA YA AIBU."
"WAKE ZAO WAWE WASTAHIVU, SIO WALEVI, SIO WAMBEA, ILA WAAMINIFU KWA KILA WAFANYALO."


"ROHO MTAKATIFU ANENA WAZIWAZI KUWA NYAKATI ZA MWISHO WENGINE KANISANI WATAJITENGA NA KUFUATA MAFUNDISHO YA KISHETANI - WAKIWAZUIA WATU WASIOE WALA KULA NYAMA - BALI MUNGU ALIVIUMBA VITU HIVI TIFURAHIKIE."
"TUMIA WAKATI WAKO NA NGUVU KATIKA MAZOEZI YA KUWA TIMAM KIROHO."
"MAZOEZI YA KIMWILI NI SAWA ILA MAZOEZI YA KIROHO NI MUHIMU ZAIDI."
"WASEMESHE KWA HESHIMA WAZEE KAMA AMBAYE NI BABA YAKO AMA VIJANA KAMA AMBAYE NI NDUGU WA KIUME WAPENDWA."
"WANAWAKE WAZEE KAMA MAMA NA WANAWAKE VIJANA KAMA NDUGU WA KIKE."
"KANISA LIWAJALI WAJANE KAMA WANAMTAZAMIA MUNGU KUWASAIDIA WALA SIO KUTANGATANGA WAKISENGENYA NA KUTAFUTA RAHA TU."
"KAMA MTU HWATAWASHUGHULIKIA JAMAA WAKE MWENYEWE, HANA HAKI KUSEMA YEYE NI MKRISTO."
"ASKOFU WAFANYAO KAZI NJEMA WALIPWE VYEMA NA KUTHAMINIWA - HASA WANAOFANYA BIDII KWA KUHUBIRI NA KUFUNZA."
"USIKUBALI MASHTAK JUU YA ASKOFU ILA KWA VINYWA VYA MASHAHIDI WAWILI AU WATATU."



"WATUMA WAKRISTO WAWATUMIKIE MABWANA WAO KWA BIDII NA KUWAHESHIMU - ISISEMEKANE KUWA WATU WA KRISTO NI WAFANYI KAZI OVYO."
"KAMA BWANA WAO NI MKRISTO, WANAPASWA KUFANYA KAZI KWA BIDII ZAIDI KWA SABABU NDUGU KATIKA KRISTO ANASAIDIKA KWA JUHUDI ZAO."
"TURIDHIKE IWAPO TUNA CHAKULA NA MAVAZI."
"WENGINE, KWA TAMAA YA PESA, HUTENDA KILA NAMNA YA MAOUVU - KWANI KUPENDA FEDHA NI MWANZO UAOELEKEA KWA KILA AINA YA DHAMBI."
"NAKUAGIZA MBELE YA MUNGU...NA MBELE YA YESU KRISTO ALIYETOA USHUHUDA MBELE YA PONTIO PILATO, UYSTIMIZE YOTE ALIYOKUAMURU UYAFANYE SASA MPAKA KUREGEA KWA BWANA WETU."
"WALIO MATAJIRI WASIJIVUNE WALA KUWEKA IMANI YAO KWENYE PESA ZAO, AMBAZO KARIBUNI ZITAISHA."
"MAJIVUNO YAO NA IMANI IWE KWNYE MUNGU ANAYEISHI ATUPAYE VITU VYOTE TUNAVYOHITAJI KWA FURAHA YETU."
WAAMBIE WATUMIE UTAJIRI WAO KUTENDA MEMA, WAWE MATAJIRI KWA MATENDO NA KUTOA KWA FURAHA KWA WALE WENYE MAHITAJI, HIVYO WAWE NA HIFADHI YA HAZINA YA KWELI MBINGUNI."


BARUA YA PILI KWA TIMOTEO ILIANDIKWA WAKATI WA KIFUNGO CHA PILI CHA PAULO HUKO ROMA.
INAWEZEKANA KUWA PAULO ALIFUNGWA TENA KAMA MOJAWAPO YA NJIA ZA NERO KUWATESA WAKRISTO.
PAULO ALIKUWA NA WASIWASI KUWA TIMOTHEO ALIKUWA ANADHOOFIKA KWA AJILI YA MATESO HUKU AKILIONGOZA KANISA LA EFESO.
ALITAKA KUMPA USUKANI WA KAZI YAKE TIMOTHEO BASI AKAMUULIZA AMTEMBELEE TENA KWA MARA YA MWISHO.
"MWANANGU TIMOTHEO, AMBAVYO NATAMANI KUKUONA TENA NIKUMBUKAVYO MACHOZI YAKO."
NAJUA WAMUAMINI MUNGU KAMA VILE MAMA YAKO EUNIKE NA BIBI YAKO LOISI."
"NATAKA KUKUKUMBUSHA UTIKISE NGUVU ZILIZO NDANI YAKO KUWA MOTO KUPITIA BARAKA YANGU NILIPOKUWEKELEA MIKONO KICHWANI MWAKO."
"KWANI ROHO MTAKATIFU HATAKI UWE MWOGA - BALI WENYE HEKIMA NA NGUVU."
"ALITUCHAGUA KWA AJILI YA KAZI HII TAKATIFU. NDIO MAANA NINATESEKA KWENYE GEREZA HILI, LAKINI SIONI HAYA KWA AJILI YAKE.
"SHIKILIA KWA NGUVU MFUMO WA UKWELI NILIOKUFUNDISHA, HASA KUHUSU IMANI NA UPENDO ANAOTAO KRISTO YESU KWAKO."


WACHANA NA MAZUNGUMZO YA KIPUMBAVU, TIMOTHEO - EPHESO NI MJI WA DIANI!
"JIPE NGUVU NA UFUNZE UKWELI HUU KWA WANAUME WAAMINIFU WAWAKAKABIDHI WENGINE - UVUMILIE TAABU KAMA ASKARI MWEMA WA YESU KRISTO."
"YESU KRISTO ALIZALIWA KATIKA FAMILIA YA MFALME DAUDI NA AKATHIBITISHA KUWA ALIKUWA MUNGU KWA KUFUFUKA KUTOKA KIFO."
"KWA KUWA NIMEHUBIRI HAYA NIMEWEKWA GEREZANI KAMA MHALIFU - LAKINI NENO LA MUNGU HALIJAFUNGWA NYORORO."
"KUWA MTENDA KAZI ASIYE TAHAYARI MUNGU ANAPOICHUNGUZA KAZI YAKO NA AWEZE KUSEMA, 'VYEMA.'"
"JIEPUSHE NA CHOCHOTE KINACHOKUPA FIKIRA ZA OUVU - LAKINI KARIBIA CHOCHOTE KINACHOKUSABABISHA KUTENDA MEMA."
"KUWA NA IMANI NA UPENDO, PAMOJA NA WALE WANAOMPENDA BWANA NA WALIO NA NYOYO SAFI."
"WATU WA MUNGU HAWAFAI KUWA NA UGOMVI; WANAPASWA KUWA WALIMU WAPOLE NA WENYE SUBIRA KWA WALE WALIOKOSEA."
"KUWA MNYENYEKEVU UNAPOJARIBU KUWAFUNZA WALIOCHANGANYIKIWA KUHUSU UKWELI."


"NYAKATI ZA MWISHO ITAKUWA VIGUMU SANA KUWA MKRISTO."
"WATU WATAJIPENDA WENYEWE, WATAPENDA FEDHA; WENYE KIBURI, WENYE KUJIVUNA, KUMDHARAU MUNGU, WASIOTII WAZAZI WAO, WASIO NA SHUKRANI NA WABAYA SANA."
"WATAWASALITI MARAFIKI ZAO; WATAKUWA WAKAIDI, KAJAWA NA MARINGO NA WAPENDAO ANASA KULIKO KUMTUKUZA MUNGU."
"WANA AKILI ZILIZOGEUKA NA WAMEIASI DINI."
"LAKINI WAJUA KUTOKA KUNITAZAMA NINAVYOAMINI NA NINAVYOISHI."
"WAJUA IMANI YANGU KATIKA KRISTO NA NILIVYOTESEKA. WAJUA NINAVYOKUPENDA NA SUBIRA YANGU."
"BALI WEWE UKAE KATIKA MAMBO ULIYOFUNDISHWA."
"TANGU UTOTO ULIFUNZWA MAANDIKO YALIYOKUPA HEKIMA YA KUOKOKA KWA KUMUAMINI KRISTO YESU."
"BIBILIA INA PUMZI YA MUNGU NA YAFAA KWA MAFUNDISHO NA KUWAONYA WATU MAKOSA YAO."
"NI NJIA YA MUNGU KUTUTAYARISHA KWA KILA NJIA - KUKAMILISHWA KUTENDA MEMA KWA WOTE."


DIANA SIO MUNGU... LAKINI YESU KRISTO NI MUNGU ALIYEKUJA DUNIANI KWA MFANO WA MWANADAMU.
"NAWASIHI MBELE YA MUNGU NA KRISTO YESU—AMBAYE SIKU MOJA ATAWAHUKUMU WALIO HAI NA WALIOKUFA—LIHUBIRI NENO LA MUNGU WAKATI WOTE, NDANI YA MSIMU NA BAADA YA MSIMU, KWA WAKATI UNAOKUFAA NA USIOKUFAA."
"UTAKUJA WAKATI AMBAO WATU HAWATASIKIZA UKWELI BALI WATATAFUTA WALIMU WATAKAOWAAMBIA WATAKACHO KUSIKIA."
"SIMAMA IMARA, USIOGOPE KUTESEKA KWA AJILI YA BWANA."
"SITAKUWA HAPA KUKUSAIDIA KW MDA MREFU - WAKATI WANGU UMEKARIBIA KUISHA."
"NIMEVIPIGA VITA VIZURI NA KUWA MUAMINIFU KWA KRISTO."
"MBINGUNI TAJI INANINGOJA AMBAYO BWANA, HAKIMU MWENYE HAKI ATANIPA SIKU HIYO."
"BALI SIO MIMI PEKE YANGU ILA KWA WOTE WANAONGOJEA KURAGEA KWAKE KWA HAMU."
"ISIPOKUWA LUKA WENGINE WAMENIACHA KWA HIYO NJOO HARAKA IWEZEKANAVYO."
"ALEXANDER YULE MFUA SHABA AMENIDHURU SANA - BWANA ATAMSHUGHULIKIA - LAKINI JITAHADHARI NAYE."
"NEEMA IWE NAWE."


TITO
BARUA KWA TITO
MWANDISHI: MTUME PAULO
TAREHE: B.K. 62-64 KATIKATI YA VIFUNGO VIWILI VYA P AULO HUKO ROMA.
TITO ALIKUWA MYUNANI ALIYEONGOZA KATIKA IMANI NDANI YA KRISTO WAKATI WA SAFARI YA KWANZA YA KIMISHONARI YA PAULO.
TITO LIMFUATA PAULO KWA BARAZA HUKO YERUSALEMU B.K. 51 KWA MADA YA KUTII SHERIA YA MUSA.
TITO ALIJIDHIHIRISHA KUWA MWANANCHI MKRISTO WA THAMANI - MWENYE MPANGILIO.
MTUME PAULO AL ALIMTUMA TITO KUTOKA EFESO HADI KORINTHO KUSAIDIA NA MGOGORO NA MFARAKANO KWENYE KANISA.
KUTOKA KORINTHO, PAULO ALIMTUMA TITO KUPANGA KUKUSANYWA KWA HELA KWA AJILI YA WAKRISTO MASIKINI HUKO YERUSALEMU.


BARUA KWA TITO HAIZINGATII KUTETEA MAFUNDISHO - PAULO ALIKUWA NA IMANI KATIKA VILE AMBAVYO TITO ALIVYOILIEWA BIBILIA NA THIOLOJIA.
MSUKUMO MKUU WA BARUA HII NI KUZIANDAA KANISA KUIPELEKA INJILI KWA WALIOPOTEA KATIKA JAMII.
ILI KUSIKIZWA KWA AJILI YA INJILI, MAANDALIZI YA MSINGI YALIKUWA KUISHI MAISHA YA UADILIFU, YENYE UPENDO, NA BILA UBINAFSI KATI YAO - KINYUME CHA WALIMU WA UONGO.
WAKATI WA KIFUNGO CHAKE CHA KWANZA KULE ROMA, PAULO ALIPITIA KWENYE KISIWA CHA KRETE KUHUBIRI.
ALIMTEUA TITO KAMA ASKOFU WA KISIWA HICHO, NA AKAMUACHA AIMALIZE KAZI.



"SABABU YANGU KUKUACHA KRETE NI KUTENGENEZA MPANGILIO WA MAMBO NA KUCHAGUA WAZEE KATIKATI KILA JIJI."
"MZEE AWE NA MWENENDO WA UTAKATIFU, MUAMINIFU KWA MKE WAKE NA MWANAMUME AMBAYE WATOTO WAKE SIO RUI WALA WASIOTII."
"WASIWE WENYE HASIRA, WALEVI, WAZUAJI VURUGU, WALA WANAOFUATA KUJIFAIDI KWA ULAGHAI."
"LAZIMA APENDE KILICHO KIZURI NA KUSHIKILIA KWA IMARA UJUMBE WA KUAMINIKA VILE ULIVYOFUNZWA - ILI AWAPE MOYO WENGINE KWA MAFUNZO IMARA NA KUWAKANA WANAOPINGA."
"KUNA WATU WENGI WAASI, WAMEJAWA NA UDANGANYIFU, HASA WAYAHUDI."
"LAZIMA WANYAMAZISHWE; WANAVURUGA JAMII NZIMA KWA KUFUNZA MAFUNZO YA UONGO - NA KWA FAIDA KUPITIA UONGO."
"HATA MOJA WA MANABII WA KRETE AMESEMA..."
WAKRETE KAWAIDA NI WAONGO, WAHUNI WAOVU NA MAKAFA WAZEMBE.
"WAKEMEE VIKALI - WANADAI WANAMJUA MUNGU, LAKINI KWA MATENDO YAO WANAMKANA."


"WAFUNZE WAZEE WA KIUME WAWE WENYE KIASI NA KUSTAHIKI HESHIMA..."
"WAZEE WA KIKE WASIWE WASINGIZIAJI WASIWE WENYE KUTUMIA MVINYO MWINGI..."
"NA VIJANA WANAUME WAWE WATULIVU."
"KATIKA MAFUNDISHO YAKO ONYESHA USAHIHI ILI YULE MWENYE KUPINGA ATAHAYARIKE KWANI HANA NENO BAYA KUSEMA JUU YETU."
"MAANA NEEMA YA BWANA IWAOKOWAYO WANADAMU WOTE IMEFUNULIWA NAYO YATUFUNDISHA KUKATAA UBAYA TUPATE KUISHI KWA KIASI, HAKI NA MAISHA YA KUMCHA MUNGU KATIKA ULIMWENGU HUU WA SASA."
"KUWA NA AMANI, MWENYE KUJALI NA WAPOLE KWA WOTE - KWA KUWA WAKATI MMOJA TULIKUWA WAASI, TUSIOTII, TUMEDANGANYWA HUKU TUKITUMIKIA KILA AINA YA TAMAA NA ANASA."
"EPUKANA NA MASWALI YA MASHINDANO NA MAGOMVI."
"MTU ALIYE MGOMVI BAADA YA KUMUONYA MARA YA KWANZA NA MARA YA PILI, MKATAE."


FILEMONI
KARIBU NA B.K. 63
FILEMONI - MOJA YA BARUA MBILI ZA GEREZANI ZILIZOANDIKWA NA MTUME PAULO.
TUKIO HILI LILIKUWA AMBAMO MTUMISHI ALIYEIBA HELA KUTOKA KWA BWANA WAKE, TAJIRI MMOJA JINA LAKE FILEMONI ALIYEISHA KATIKA MJI WA KOLOSAI.
KAMA WATUMWA WENGINE WENGI, ONESIMO ALIKIMBIA KWENDA ROMA.
ILITOKEA, ALIVYOKUWA ROMA, ALIKUTANA NA PAULO NA MTUME AKAMUONGOZA ONESIMO KWA IMANI KATIKA KRISTO.
INGAWA HAKUWA MFUNGWA ONESIMO ALIMSAIDIA PAULO ALIPOKUWA GEREZANI.
PAULO ALIKUWA ANATUMA BARUA KWA WAKOLOSAI KUPITIA TIKIKO - PIA BARUA HII KWA FILEMONI


TIKIKO, NIPE NGOZI NA KALAMU TAFADHALI.
PAULO ALIITUMIA FURSA HII KUFUNZA KANISA KUHUSU MSAMAHA NA KUREJESHA UPYA UHUSIANO KATI YA WANAUME WAWILI.
PAULO AKIWA GEREZANI KWA KUHUBIRI HABARI NJEMA KUMHUSU YESU KRISTO, NA KUTOKA NDUGU TIMOTHEO.
KWA FILEMONI NA KWA KANISA ILIYO NYUMBANI KWAKO, MUNGU BABA YETU NA BWANA YESU KRISTO AKUPE BARAKA NA AMANI.
"NAMSHUKURU MUNGU SIKU ZOTE KWA SABABU NASKIA KUHUSU UPENDO WAKO KWA BWANA YESU NA WATU WAKE."
"NAOMBA UNAPOSHIRIKI KWA IMANI YAKO WENGINE WATAONA UZURI UTOKAO KUTOKA KUMJUA KRISTO YESU."
MIMI NA WENGINE WENGI TUMEPATA FURAHA NA FARAJA KUTOKA KWA UPENDO NA UKARIMU WAKO.
MIMI, PAULO, MZEE ALIYE GEREZANI KWA AJILI YA KRISTO NATAKA KUKUOMBA JAMBO MOJA.
"NINGEKUAGIZA KWA JINA LA KRISTO KWA SABABU NDICHO KITU SAWA KUFANYA LAKINI NAPENDELEA KUULIZA KWA UPENDO."


" NAKUSIHI UMUONYESHE UKARIMU MWANANGU ONESIMO AMBAYE NILIMLETA KWA BWANA HAPA KWENYE MINYOROR YANGU."
"HAKUWA NA MAANA KWENU HAPO AWALI - LAKINI SASA ATATUFAA SOTE.
NAMTUMA - MOYO WANGU - ARUDI KWENU.
NILITAKA KUMUEKA HAPA NAMI ILI UNGALISAIDIA KUPITIA KWAKE - ILA SIKUTAKA KUFANYA HIVYO BILA RUHUSA YAKO.
IWAZE HIVI - ALITOROKA KWA MDA MFUPI ILI SASA AWE WAKO MILELE - SIO KAMA MTUMWA LAKINI AFADHALI ZAIDI - NDUGU YAKO.
"SASA ATAKUWA NA MAANA ZAIDI KWAKO PIA KWA SABABU SIO MTUMWA TU ILA NDUGU YAKO KATIKA KRISTO."


"KAMA KWELI MIMI NI RAFIKI YENU, MKARIBISHE AMBAVYO MNGENIKARIBISHA MIMI."
"KAMA AMEWADHURU AU KUWAIBIA NILIPISHE MIMI - NITAWALIPA."
"MIMI, PAULO, NAWAHAKIKISHIA, ILA SITATAJA NI MANGAPI NINAYOWADAI!"
"UKWELI NI KWAMBA - HATA MNADAIWA NAMI ROHO ZENU HASWA!"
"NDUGU MPENDWA, NIPE FURAHA NA KITENDO HICHI HA UPENDO NA MOYO WANGU MCHOVU UTAMSIFU BWANA."
"NIMEKUANDIKIA BARUA HII MAANA NINA HAKIKA UTAFANYA NINAYOKUOMBA NA HATA ZAIDI!"
MTUME WA BWANA WETU ATUMAINI KUACHILIWA TOKA GEREZANI HIVI KARIBUNI NA AOMBA TUMTAYARISHIE CHUMBA.
ALAFU... TUMPOKEE TENA ONESIMO KAMA NDUGU.
"BARAKA ZA BWANA WETU YESU KRISTO ZIWE JUU YA ROHO YAKO."
"PAULO"

"THE BIBLE EXPLAINED
IN EVERY LANGUAGE."





**SUPERBIBLE.TV**